# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**MUHTASARI WA**

# SAYANSI JAMII

**KWA SKULI ZA MSINGI**

**DARASA LA I -IV**

**2009**

**© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2009**

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa au kutoa muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

**Umetayarishwa na :**
**IDARA YA MITAALA NA MITIHANI**
**S.L.P 3070.**
**ZANZIBAR.**

# YALIYOMO

**Ukurasa**

**UTANGULIZI** .......... iv
Sababu za Kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi .......... iv
Umuhimu wa Somo la Sayansi Jamii .......... v
Madhumuni ya Elimu Zanzibar .......... vi
Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi .......... vi
Ujuzi wa Jumla katika Somo la Sayansi Jamii .......... vii
Malengo ya Jumla ya Somo la Sayansi Jamii .......... viii
Uchaguzi na Mpangilio wa Mada .......... viii
Muundo wa Muhtasari .......... x
**DARASA LA KWANZA** .......... 1
UJUZI .......... 1
MALENGO .......... 1
**DARASA LA PILI** .......... 18
UJUZI .......... 18
MALENGO .......... 18
**DARASA LA TATU** .......... 32
UJUZI .......... 32
MALENGO .......... 32
**DARASA LA NNE** .......... 45
UJUZI .......... 45
MALENGO .......... 45

## UTANGULIZI

Muhtasari huu ni wa somo jipya la Sayansi Jamii, ambalo katika mtaala mpya (2009) litafundishwa katika Darasa la I hadi IV. Katika mtaala wa 1998 ambao umedumu hadi 2009, mada za somo la Sayansi Jamii zilikuwa zikifundishwa kwa Darasa la I - III katika somo la Mazingira na Darasa la IV – VII katika somo la Sayansi Jamii. Katika utangulizi huu unatolewa ufafanuzi wa sababu za kuandika mtaala mpya, maudhui ya somo hili na umuhimu wake katika mtaala wa elimu ya msingi. Vile vile kuna Madhumuni ya Elimu Zanzibar; Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar; Ujuzi wa jumla wa somo unaotarajiwa kuoneshwa na walengwa; Malengo ya jumla ya kufundisha somo hili na uchaguzi na mpangilio wa mada. Mwishoni mwa utangulizi kuna ufafanuzi wa vipengele vya jadweli za ufundishaji na ujifunzaji.

### Sababu za Kuandika Mtaala Mpya wa Elimu ya Msingi.

Mnamo mwaka 2008/2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliendesha mchakato wa kufanya mapitio, kufupisha na kuandika upya mtaala wa elimu ya msingi. Madhumuni yalikuwa ni kufanya mtaala ushabihiane na Sera ya Elimu ya Zanzibar (2006). Sera hii inalenga kurekebisha ubora na muundo wa elimu ya msingi; kuweka muunganiko bayana kati ya elimu ya msingi, maandalizi na sekondari ili kukidhi matarajio ya walengwa na jamii yao. Sera ya Elimu ya 2006 imebadili muundo wa elimu kwa kutamka kuwa elimu ya maandalizi itakuwa ni sehemu ya elimu ya lazima, elimu ya msingi itakuwa ni ya miaka sita (6) badala ya saba (7) na baadhi ya masomo ya ngazi ya msingi yatafundishwa kwa kutumia lugha ya Kiingereza kwa madarasa ya Tano na Sita.

Mambo mengine yaliyochochea mapitio ni pamoja na haya yafuatayo:

- Mwelekeo wa kilimwengu katika maendeleo ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia.
- Mwitiko wa serikali kwa Wanzanzibari kudai nafasi zaidi za skuli kwa watoto wote na kuongeza ubora wa elimu inayotolewa.
- Mwitiko wa serikali kwa matokeo ya Utafiti wa Mahitaji katika Mtaala wa Elimu ya Msingi wa 2008.

Uatafiti wa 2008 ilizingatia mapungufu yafuatayo katika mtaala wa 1998:

- Haukukuza stadi za kuwasiliana, ubunifu na fikra yakinifu.
- Kuwa haukuzingatia vya kutosha mahitaji ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu na masuala mtambuka.
- Ulihimiza matumizi ya mbinu za kufundishia/kujifunzia zilizojikita kwa mwalimu zaidi kuliko kwa mwanafunzi.
- Ufundishaji/ujifunzaji ulikuwa wa kinadharia zaidi kuliko kuwa wa vitendo au ushiriki wa wanafunzi.

Kutokana na changamoto kama hizo, serikali ilifanya maamuzi kadhaa ya msingi kuhusu mtaala wa Elimu ya Msingi. Mojawapo ni kubuni masomo mapya ili elimu iendane na wakati na kuakisi matakwa na matarajio ya walengwa na jamii yao. Uamuzi mwengine ni kuweka muunganiko bayana baina ya mtaala wa elimu ya maandalizi, msingi pamoja na mtaala wa sekondari. Hii ililenga kuepuka kurudia rudia mada.

**Umuhimu wa Somo la Sayansi Jamii**

Sayansi Jamii huhusu kujifunza juu ya watu na mazingira wanamoishi. Mazingira yamesheheni rasilimali ambazo hutuwezesha kuishi. Tunavyoishi na kufanya shughuli anuai pamoja huwa tunaunda mifumo inayotuunganisha. Kwa hiyo somo la Sayansi Jamii lina madhumuni ya kuwapatia wanafunzi maarifa, stadi, mwenendo na maadili bora ili kuwawezesha kuishi sawia katika mazingira yao. Vile vile litawawezesha kuishi kama raia welevu na wanaoweza kushiriki kwenye masuala ya kijamii, kitaifa na kilimwengu. Aidha litawawezesha kutambua kuwa mazingira yao au ulimwengu unabadilika. Utawaonesha muachano wa mitindo ya maisha na maoni ya mawazo. Yote haya yatawawezesha kutathmini, kubadili au kukumbatia imani au mitindo yao ya maisha.

Inaaminika kwamba kupitia somo hili wanafunzi watafahamu uhusiano kati ya chanzo na athari au matokeo ya masuala ya kijamii. Watajenga tabia ya kuheshimu majukumu yao pamoja na mali ya jamii yao. Hili litawawezesha kuishi kwa amani kama raia wenye faida kwa jamii. Litawapatia stadi za kutatua matatizo kwa tija, kufanya maamuzi kwa busara, kutathmini uzito wa masuala yanayowakabili na kufanya uamuzi unaostahiki.

**Madhumuni ya Elimu Zanzibar**

Yafuatayo ndiyo madhumuni ya elimu Zanzibar:

1. Kukuza na kudumisha tabia na desturi bora za Wazanzibari na Watanzania ili kuimarisha umoja na utambulisho wao wa kiutamaduni.
2. Kuimarisha upatikanaji na matumizi sahihi ya aina mbalimbali za maarifa, stadi na mwelekeo/mwenendo kwa ajili ya kuendeleza kikamilifu utu na ubora wa maisha ya jamii.
3. Kuwezesha kila mwananchi kuelewa na kuheshimu misingi ya Katiba ya Zanzibar na ya Tanzania, Haki za Binadamu, pamoja na haki, wajibu na majukumu ya kiraia.
4. Kuendeleza na kuhimiza matumizi bora, uangalizi na utunzaji wa mazingira.
5. Kukuza utashi na heshima ya kufanya kazi za kujiajiri na kuajiriwa pamoja na nidhamu kazini na utendaji kazi kwa kiwango cha juu cha ubora.
6. Kukuza na kudumisha misingi ya kuvumiliana, amani, upendo, haki, maelewano, haki za binadamu na uhuru, umoja wa kitaifa na kimataifa kama vinavyofafanuliwa katika mikataba ya kimataifa.

**Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi**

Yafuatayo ndiyo madhumuni na malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar:

1. Kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda skuli kujenga na kudumisha misingi imara ya stadi za kusoma, kuandika, kuhesabu, ubunifu na mawasiliano kwa lugha za Kiswahili, Kiingereza na lugha nyengine za kigeni.

2. Kuwezesha wanafunzi kuelewa matumizi ya sayansi na teknolojia na kutambua mchango wake katika maendeleo ya taifa lao na ulimwengu.
3. Kuweka, kuendeleza na kudumisha miongoni mwa wanafunzi misingi imara ya stadi za kufikiri na udadisi ili kuelewa mazingira yao na mahusiano ya kijamii.
4. Kuwezesha wanafunzi kuelewa jinsi matukio yaliyopita yanavyoathiri matukio ya wakati uliopo na ya wakati ujao.
5. Kugundua vipaji vya kila mwanafunzi kuanzia umri mdogo ili kuvidumisha na kuviendeleza.
6. Kuweka misingi imara ya stadi za uchunguzi fikra na ushirikiano katika kutatua matatizo yanayodumaza maendeleo binafsi ya wanafunzi na ya jamii yao.
7. Kuwaandaa wanafunzi kujiunga na elimu ya sekondari.
8. Kuwezesha wanafunzi kukuza uwezo wao kiakili na utashi wa kujitafutia maarifa.
9. Kuwazoesha wanafunzi shughuli za uzalishaji mali na kukuza ari yao katika kutekeleza majukumu ya kijamii.
10. Kuwezesha wanafunzi kutambua na kuenzi umoja wa taifa lao pamoja na ushirikiano baina ya taifa lao na watu na mataifa mengine.
11. Kuwezesha wanafunzi kujenga maadili mema kiroho, kiutamaduni na kiitikadi ili kukuza uzalendo na ufahamu wa hali ya nchi yao kihistoria, kisiasa na kijamii.
12. Kukuza na kudumisha nidhamu binafsi ya wanafunzi, kuheshimu usawa wa kijinsia na kulinda afya zao na za watu wengine.
13. Kuwezesha wanafunzi kujenga tabia za umaridadi na unadhifu pamoja na matumizi bora ya muda wao wa mapumziko.
14. Kukuza upendo wa wanafunzi kwa mazingira wanamoishi pamoja na utashi wa kuyatunza.

**Ujuzi wa Jumla katika Somo la Sayansi Jamii**

Mtaala huu umejikita katika kumpatia ujuzi mwanafunzi (badala ya kujikita katika kufundisha maudhui tu). Ujuzi ni muunganiko sawia wa maarifa, stadi na mwenendo/mwelekeo anavyotarajiwa kuupata mwanafunzi.

Baada ya kujifunza somo la Sayansi Jamii katika skuli za msingi wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kuchunguza na kutafakari matukio ya wakati uliopita na uliopo ili kujielimisha na kushiriki katika maendeleo ya jamii.
2. Kubainisha mamlaka zilizopo na kushiriki katika kupata viongozi bora.
3. Kueleza asili ya Taifa lao na kuainisha sifa zinazowatambulisha kama Wazanzibari na kama Watanzania.
4. Kubainisha na kuheshimu alama za nchi ya Zanzibar na serikali yake pamoja na za Taifa la Tanzania na serikali yake.
5. Kuonesha dalili za uadilifu na uzalendo katika mahusiano na shughuli zao za kila siku.
6. Kubainisha na kuepuka mambo yanayohatarisha usalama wao na utu wao ili kujenga ustawi wao na wa jamii.
7. Kuyahifadhi na kuyatumia mazingira yao kwa njia endelevu kwa faida yao na Taifa.
8. Kubainisha haki zao na za wengine na mambo yanayoziathiri, kuzitetea na kutekeleza wajibu wao ipasavyo.
8. Kutumia stadi za kutafuta maarifa na stadi za kisayansi jamii kutoka katika maktaba na vifaa vya TEHAMA.

**Malengo ya Jumla ya Somo la Sayansi Jamii**

Somo la Sayansi Jamii linafundishwa katika skuli za msingi ili kuwezesha wanafunzi:-

1. Kuelewa historia na utamaduni wa Zanzibar katika nyakati mbali mbali pamoja na maelezo yake.
2. Kufahamu mazingira yanayowazunguka pamoja na uhifadhi wake.
3. Kuelewa mambo yanayotishia usalama wao na uepukaji wake kwa minajili ya kukuza ustawi wao na wa jamii yao.
4. Kujitambua kama Wazanzibari na Watanzania, kukuza maadili na uhusiano mwema.
5. Kuzitambua njia za upatikanaji wa viongozi, kuwaheshimu na kuziheshimu mamlaka zilizopo.
6. Kuelewa utetezi wa haki zao kama watoto na utekelezaji wa wajibu wao.
7. Kuwa na tabia ya usomaji katika maktaba na utumiaji wa vifaa vya TEHAMA kwa upataji wa maarifa mapya na stadi za kisayansi jamii.

**Uchaguzi na Mpangilio wa Mada**

Katika kuchagua mada zimezingatiwa zile ambazo wakati wa kuzifundisha/kujifunza zitawapatia wanafunzi maarifa, stadi na mwenendo kama vilivyoelezwa hapo juu. Zimezingatiwa pia mada za masuala mtambuka za Haki za Mtoto na maadili mema. Aidha kuna mada za stadi za maisha, hususani, uhimili wa mhemko na shinikizo –rika. Mada zimepangwa kimantiki ili wanafunzi wa Darasa la I waanze kwa kufundishwa/kujifunza mada rahisi. Kadiri wanavyopanda madarasa watajifunza mada ngumu na tata. Zifuatazo ndizo mada zilizochaguliwa na kupangwa katika madarasa ya I – IV.

| NA. | MADA KUU | DARASA I | DARASA II | DARASA III | DARASA IV |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Familia Yetu, Ukoo Wetu | √ | √ | √ | √ |
| 2. | Skuli Yetu | √ | √ | √ | √ |
| 3. | Utamaduni wa Zanzibar | √ | √ | √ | √ |
| 4. | Mazingira Yetu | √ | √ | √ | √ |
| 5. | Usalama | √ | √ | - | √ |
| 6. | Uzalendo | √ | √ | √ | √ |
| 7. | Maadili | √ | √ | √ | √ |
| 8. | Mzanzibari na Mtanzania | √ | √ | √ | √ |
| 9. | Haki na Wajibu wa Mtoto | √ | √ | √ | √ |
| 10. | Alama za Utambulisho wa Kitaifa | - | - | √ | √ |

## Muundo wa Muhtasari

Muhtasari huu una sehemu kuu mbili: Kurasa za mwanzo na Jadweli za Ufundishaji na Ujifunzaji.

## Kurasa za Mwanzo

Sehemu hii inajumuisha jalada, ukurasa wa jina la muhtasari, ukurasa wa haki-miliki na wa yaliyomo. Vilevile, kuna maelezo ya sababu za kuandika mtaala mpya (2009) na maelezo ya umuhimu wa somo hili.. Kisha kuna Madhumuni ya Elimu Zanzibar; Madhumuni na Malengo ya Elimu ya Msingi Zanzibar; Ujuzi wa Jumla na Malengo ya Jumla katika Somo la Sayansi Jamii pamoja na uchaguzi na mpangilio wa mada.

## Jadweli ya Ufundishaji na Ujifunzaji

Sehemu hii inahusu taratibu za ufundishaji na ujifunzaji na imegawika kwa madarasa ya I hadi la IV. Muhtasari wa kila darasa umetanguliwa na orodha ya ujuzi ambao wanafunzi wanatakiwa kuonesha baada ya kujifunza/kufundishwa somo hili katika darasa husika. Kisha kuna orodha ya malengo ya kujifunza/kufundisha somo hili katika darasa husika. Baada ya orodha ya malengo linafuata jadweli la ufundishaji/ujifunzaji lenye safu-wima sita zenye vichwa vya: Mada Kuu/Mada Ndogo, Malengo Mahsusi; Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia, Vifaa/Zana; Upimaji na Vipindi. Yafuatayo ni maelezo ya yaliyomo katika safu-wima za jadweli ya ufundishaji/ujifunzaji.

### *Mada Kkuu/Mada Ndogo*

Mada hutamka maudhui yatakayofundishwa. Chini ya mada kuna mada ndogo ambazo huonesha kina na mawanda ya ufundishaji/ujifunzaji wa mada husika.

***Malengo Mahsusi***

Kila mada ndogo imeandikiwa lengo au malengo mahsusi. Hayo yanaeleza stadi, mwenendo/mwelekeo na maarifa ambayo kila mwanafunzi anapaswa kujifunza katika mada ndogo husika. Malengo mahsusi ndiyo yanatumiwa kufanyia upimaji. Aidha ufikiaji wa malengo mahsusi katika kujifunza hutafsiriwa kama ufikiaji wa stadi, mwelekeo na maarifa yanayolengwa katika mada husika. Kila mwanafunzi anatakiwa kuyafikia malengo mahsusi yaliyotajwa. Hivyo, mwalimu anatakiwa kuhakikisha kuwa lugha ya alama inatumika kumfundisha mwanafunzi kiziwi na maandishi ya Braille au zana mguso zinatumika kwa mwanafunzi asiyeona. Taratibu, miongozo, vifaa na mbinu za kufundishia/kujifunzia kwa makundi mengine ya watoto wenye mahitaji maalum zitumike ipasavyo.

***Mbinu za Kufundishia/Kujifunzia***

Safu wima hii inaonesha baadhi ya mbinu zinazofaa kufundishia/kujifunzia. Ni mbinu shirikishi tu zinazopendekezwa. Hii ni kwa sababu zinahimiza wanafunzi kujitafutia maarifa na kujenga maana kwa kile wanachojifunza. Mbinu hizo ni kama vile majadiliano ya vikundi; maigizo; nyimbo; changanyakete; bungua-bongo; ziara za kielimu, kumwalika mgeni na nyingine ambazo mwalimu anaweza kuzitumia kutegemea mazingira, mada na umri wa wanafunzi. Mbinu zilizomo katika safu hii ni mapendekezo tu. Mwalimu anashauriwa atumie mbinu nyingine anazozimudu zitakazoshirikisha wanafunzi na kufanikisha ufundishaji/ujifunzaji.

***Vifaa/Zana***

Safu – wima hii inaonesha vifaa au zana zinazofaa kutumia katika kufundisha/kujifunza kwa kila mada. Kumbuka kuwa kitabu cha kiada na kiongozi cha mwalimu ni zana muhimu katika kufundisha/kujifunza somo husika. Mwalimu anashauriwa kuzitumia hizi pamoja na nyengine atakazoona zinafaa au zinapatikana katika mazingira yake. Mwalimu anashauriwa kubuni na kutengeneza zana/vifaa kulingana na upatikanaji wa malighafi zinazopatikana katika mazingira yake. Aidha mwalimu anashauriwa kuhimiza wanafunzi kufaragua, kubuni na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia kila inapowezekana.

***Upimaji***

Safu hii inaonesha maelekezo ya upimaji wa wanafunzi. Mwalimu hana budi kupima maendeleo ya wanafunzi wake. Hii itamwezesha kujua uwezo na matatizo ya wanafunzi, ubora wa mbinu za kufundishia/kujifunzia anazozitumia na ubora wa zana/vifaa anavyotumia. Vile vile upimaji humwezesha mwalimu kupanga na kutekeleza mikakati ya kuwasaidia wanafunzi wazito. Aidha, upimaji humwezesha mwalimu kupendekeza marekebisho ya mtaala na vitabu vya kufundishia/kujifunzia. Upimaji wa mwisho wa muhula au mwaka huonesha kiwango cha ujuzi alichofikia mwanafunzi. Kwa sababu hizo, mwalimu anashauriwa kupima maendeleo ya mwanafunzi kila siku, kila mwezi, kila muhula na kila mwaka kwa kuzingatia malengo mahsusi ya kila mada iliyofundishwa na njia mwafaka za upimaji.

***Vipindi***

Safu wima hii inaonesha makadirio ya idadi ya vipindi vya kufundisha/kujifunza kila mada. Idadi hiyo imefikiwa baada ya kujumlisha idadi ya vipindi vya siku 224 za mwaka wa masomo na kuvigawa kwa idadi ya mada ndogo zinazounda muhtasari. Makadirio haya ya vipindi yanaweza kubadilika kulingana na mazingira ya ufundishaji/ujifunzaji. Utawala wa skuli unahimizwa kufidia muda wa masomo utakaopotea kutokana na dharura za sikukuu za kidini au za kiserikali.

Somo la Sayansi Jamii lina vipindi vinne (4) kwa wiki katika darasa la I, II, III na IV. Muda wa kipindi kimoja kuanzia Jumatatu hadi Alhamisi ni dakika 40 kwa shifti ya asubuhi; utakuwa ni dakika 35 kwa shifti ya mchana. Siku za Ijumaa muda wa kila kipindi utakuwa dakika 30 tu.

**KATIBU MKUU**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI**

**ZANZIBAR**

## DARASA LA KWANZA

**UJUZI**

Baada ya kujifunza somo la Sayansi Jamii katika Darasa la I wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kuelezea historia ya familia zao na kuboresha majukumu ya wanafamilia.
2. Kuonesha heshima kwa uongozi wa nyumbani na kutekeleza majukumu wanayopewa.
3. Kuainisha na kutaja vitu vinavyomtambulisha Mzanzibari na Mtanzania.
4. Kuainisha na kufuata alama za barabarani na kutumia barabara kwa uangalifu.
5. Kubainisha na kuepuka mambo yanayohatarisha usalama wao ndani ya jamii.
6. Kubainisha rasilimali zilizopo kwenye mazingira yanayowazunguka na kuzitumia ipasavyo.
7. Kufahamu na kuainisha haki wanazostahiki kupewa na kutekeleza wajibu wao kama watoto.
8. Kutumia maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kupata maarifa, stadi za kisayansi jamii.

**MALENGO**

Malengo ya kufundisha somo la Sayansi Jamii katika Darasa la I ni kuwezesha wanafunzi:-

1. Kufahamu maelezo ya historia ya familia zao na majukumu ya wanafamilia.
2. Kufahamu vitu vilivyopo katika mazingira yao na matumizi yake endelevu.
3. Kufahamu mambo yanayotishia usalama wao barabarani na maelezo yake.
4. Kuzitambua alama za barabarani, tafsiri yake pamoja na matumizi ya barabara kwa uangalifu.
5. Kuzitambua na kueleza sifa na utambulisho wa Mzanzibari na Mtanzania pamoja na maelezo yake.
6. Kuwatambua na kuwaheshimu viongozi wa nyumbani na utekelezaji wa majukumu yao ya nyumbani wakiwa kama watoto.
7. Kutambua mambo mema ambayo mtoto hupaswa kutendewa nyumbani na maelezo yake.
8. Kufahamu utekelezaji wa majukumu yao ya nyumbani kama watoto.
9. Kupata stadi za matumizi ya maktaba na vifaa vingine vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kisayansi jamii.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. **FAMILIA YETU, UKOO WETU**. a) Maana ya Familia. | Mwanafunzi aweze: (i) Kueleza maana ya familia. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya familia. | 1. Chati inayoonesha wanafamilia. 2. Chati mguso inayoonesha wanafamilia.. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya familia? | 14 |
| | (ii) Kutaja watu wanaoishi katika familia yake. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu,mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja watu wanaoishi katika familia yake kuanzia kiongozi mkuu. | 1. Chati inayoonesha wanafamilia. 2. Chati mguso inayoonesha wanafamilia. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja watu wanaoishi katika familia yake? | |
| | (iii) Kuchora mchoro unaoonesha wanafamilia. | Kwa kutumia mbinu ya kuchora, mwalimu awaongoze wanafunzi kuchora mchoro unaoonesha wanafamilia. | 1. Chati inayoonesha wanafamilia. 2 Chati mguso inayoonesha wanafamilia. | Je, mwanafunzi anaweza kuchora mchoro unaoonesha wanafamilia? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Chimbuko la Familia. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja waanzilishi wa familia yake upande wa baba. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja waanzilishi wa familia yake upande wa baba. | 1. Chati inayoonesha familia yake upande wa baba.<br>2. Chati mguso inayoonesha familia yake upande wa baba.. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja waanzilishi wa familia yake upande wa baba? | 10 |
| | (ii) Kutaja waanzilishi wa familia yake upande wa mama. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja waanzilishi wa familia yake upande wa mama. | 1. Chati inayoonesha familia yake upande wa mama.<br>2. Chati mguso inayoonesha familia yake upande wa mama. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja waanzilishi wa familia yake upande wa mama? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Mahitaji ya Familia Zama za Kale na Sasa. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja mahitaji ya familia ya zama za kale. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mahitaji ya familia ya zama za kale. | 1. Orodha yenye mahitaji ya familia ya zama za kale.<br>2. Orodha katika maandishi ya Braille yenye mahitaji ya familia ya zama za kale. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mahitaji ya familia ya zama za kale? | 10 |
| | (ii) Kutaja mahitaji ya familia ya hivi sasa. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mahitaji ya familia ya hivi sasa. | 1. Orodha yenye mahitaji ya familia ya hivi sasa.<br>2. Orodha katika maandishi ya Braille yenye mahitaji ya familia ya hivi sasa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mahitaji ya familia ya hivi sasa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| d) Kazi za Wanafamilia Zama za Kale na Sasa. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza kazi za wanafamilia zama za kale. | Kwa kutumia mbinu ya masimulizi ya hadithi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kazi za wanafamilia zama za kale. | 1.Chati inayoonesha zana zilizotumika zama za kale.<br>2.Chati mguso inayoonesha zana zilizotumika zama za kale. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kazi za wanafamilia zama za kale? | 8 |
| | (ii) Kueleza kazi za wanafamilia hivi sasa. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kazi za wanafamilia hivi sasa. | 1. Orodha inayoonesha zana zinazotumia hivi sasa.<br>2. Orodha katika maandishi ya Braille inayoonesha zana zilizotumika hivi sasa. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza kazi za wanafamilia hivi sasa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| e) Kusambaratika kwa Familia. | Mwanafunzi aweze:<br>i) Kutaja sababu za kusambaratika kwa familia. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja sababu zinazopelekea kusambaratika kwa familia. | - | Je, mwanafunzi anaweza kutaja sababu zinazopelekea kusambatatika kwa familia? | 5 |
| | ii) Kueleza athari zinazotokana na kusambaratika kwa familia. | Kwa kutumia mbinu ya kisa mkasa, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari zinaotokana na kusambaratika kwa familia. | - | Je, mwanafunzi anaweza kueleza athati zinazotokana na kusambaratika kwa familia? | |
| 2**. SKULI YETU**<br>a) Historia ya Skuli. | Mwanafunzi aweze kueleza historia ya skuli yake. | Kwa kutumia mbinu ya utafiti, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza taarifa za historia ya skuli yao. | 1. Bango linaloonesha historia ya skuli yao.<br>2. Bango mguso linaloonesha historia ya skuli yao.<br>3. Mafaili ya skuli yenye | Je, mwanafunzi anaweza kueleza historia ya skuli yake? | 6 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | kumbukumbu za historia ya skuli yao.<br>4. Mafaili ya skuli yenye kumbukumbu za historia ya skuli yao katika maandishi ya Braille. | | |
| b) Mipaka ya Skuli. | Mwanafunzi aweze kubainisha vitu vilivyopakana na skuli yake. | Kwa kutumia mbinu ya matembezi ya kimafunzo mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha vitu vilivyopakana na skuli yake. | 1. Ramani ya skuli inayoonesha ujirani wake.<br>2. Ramani mguso ya skuli inayoonesha ujirani wake.<br>3. Picha zinazoonesha vitu vilivyopakana na | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha vitu vilivyopakana na skuli yake? | 6 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | skuli yao.<br>4. Mazingira halisi.<br>5. Picha mguso zinazoonesha vitu vilivyopakana na skuli yao. | | |
| **3. UTAMADUNI WA MZANZIBARI**<br>a) Michezo ya Asili ya Watoto wa Kizanzibari. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutaja michezo ya asili ya watoto wa Kizanzibari. | Kwa kutumia mbinu ya utafiti, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja michezo ya asili ya watoto wa Kizanzibari na taratibu zake. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Kitabu cha kiada<br>3. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja michezo ya asili ya watoto wa Kizanzibari? | 12 |
| | ( ii) Kucheza michezo ya asili ya watoto wa Kizanzibari. | Kwa kutumia mbinu ya michezo, mwalimu awaongoze wanafunzi kucheza michezo ya asili ya watoto wa Kizanzibari. | Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kucheza michezo ya asili ya watoto wa Kizanzibari? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Hadithi za Watoto na Vitendawili | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kusimulia hadithi fupi fupi za watoto. | Kwa kutumia mbinu burudiko, mwalimu awaongoze wanafunzi kusimulia hadithi fupi fupi za watoto. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Vitabu vya hadithi za watoto.<br>3. Vitabu vya hadithi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kusimulia hadithi fupi fupi za watoto? | 16 |
| | (ii) Kueleza mafundisho ya hadithi husika. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza mafundisho ya hadithi husika. | Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza mafundisho ya hadithi husika? | |
| | (iii) Kutega na kutegua vitendawili. | Kwa kutumia mbinu burudiko, mwalimu awaongoze wanafunzi kutenga na kutegua vitendawili. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Kitabu cha kiada.<br>3. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutega na kutegua vitendawili? | |
| | (iv) Kutoa maana ya vitendawili. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kutoa maana ya vitendawili. | Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kutoa maana ya vitendawili? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **4. MAZINGIRA YETU**<br><br>Vitu katika Mazingira Yetu. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kubainisha vitu vilivyomo katika mazingira. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha vitu vilivyomo katika mazingira. | 1. Picha za vitu vilivyomo katika mazingira. Mfano: miti, wanyama na majengo.<br>2. Picha mguso za vitu vilivyomo katika mazingira.<br>3. Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha vitu vilivyomo katika mazingira? | 12 |
| | (ii) Kueleza manufaa ya vitu vilivyomo katika mazingira. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza manufaa ya vitu vilivyomo katika mazingira. | 1. Picha za vitu vilivyomo katika mazingira<br>2. Picha mguso ya vitu vilivyomo katika mazingira. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza manufaa ya vitu vilivyomo katika mazingira? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (iii) Kueleza athari za uharibifu wa vitu vilivyomo katika mazingira. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza athari za uharibifu wa vitu vilivyomo katika mazingira. | 1. Picha za vitu vilivyomo katika mazingira.<br>2. Mazingira halisi.<br>3. Picha mguso za vitu vilivyomo katika mazingira. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza athari za uharibifu wa vitu vilivyomo katika mazingira? | |
| **5. USALAMA**.<br>a) Alama za Barabarani. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kutafsiri maana ya alama za barabarani. | Kwa kutumia mbinu ya uchunguzi, mwalimu awaongoze wanafunzi kutafsiri maana ya alama za barabarani. | 1. Chati inayoonesha alama za barabarani.<br>2. Chati mguso inayoonesha alama za barabarani.<br>3. Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kutafsiri maana ya alama za barabarani? | **7** |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuziheshimu ipasavyo alama za barabarani. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha jinsi ya kuziheshimu ipasavyo alama za barabarani. | 1. Chati inayoonesha alama za barabarani.<br>2. Chati mguso kwa wasioona.<br>3. Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kuziheshimu ipasavyo alama za barabarani? | |
| | (iii) Kuzitumia ipasavyo alama za barabarani. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya vitendo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuzitumia ipasavyo alama za barabarani. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Vipeperushi kuhusu usalama barabarani.<br>4. Vipeperushi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuzitumia ipasavyo alama za barabarani | |
| b) Usalama Barabarani. | Mwanafunzi aweze kufuata kanuni za kutumia barabara. | Kwa kutumia mbinu ya kualika mgeni mwalimu awaongoze wanafunzi kufuata kanuni za kutumia barabara. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Vipeperushi.<br>3. Vipeperushi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kufuata kanuni za kuzitumia barabara? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | 4. Kitabu cha kiada.<br>5. Kitabu cha kiada Katika maandishi ya Braille. | | |
| c) Mambo Yanayotishia Usalama Barabarani. | (i) Kutaja mambo yanayotishia usalama barabarani. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja mambo yanayotishia usalama barabarani. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Vipeperushi vya usalama barabarani<br>3. Vipeperushi katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mambo yanayotishia usalama barabarani? | 9 |
| | (ii) Kuepuka mambo yanayotishia usalama barabarani. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kuepuka mambo yanayotishia usalama barabarani. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada Katika maandishi ya Braille. | Je,mwanafunzi anaweza kuepuka mambo yanayotishia usalama barabarani? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **6. UZALENDO** Heshima na Utii Kwa Uongozi wa Nyumbani. | Mwanafunzi aweze: (i) Kutaja uongozi wa nyumbani kwao. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja uongozi wa nyumbani kwao. | 1. Kitabu cha kiada. 2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je,mwanafunzi anaweza kutaja uongozi wa nyumbani kwao? | 9 |
| | (ii) Kuonesha namna ya kuheshimu viongozi wa nyumbani kwao . | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuigiza namna ya kuheshimu viongozi wa nyumbani kwao. | 1. Vifaa vinavyotumika kufanya igizo. 2. Kitabu cha kiada. 3. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuonesha namna ya kuheshimu viongozi wa nyumbani kwao? | |
| **7. MAADILI.** a) Kujiheshimu. | Mwanafunzi aweze: i) Kubainisha njia za kujiheshimu zinazokubalika katika jamii | Kwa kutumia mbinu ya kisa mkasa, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha njia za kujiheshimu zinazokubalika katika jamii. | | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha njia za kujiheshimu zinazokubalika katika jamii? | 4 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| . | ii) Kuonesha kwa vitendo njia za kujiheshimu zinazokubalika katika jamii. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha kwa vitendo, njia za kujiheshimu zinazokubalika katika jamii. | 1.Vifaa vinavyotumika kufanyia igizo.<br>2.Picha za vitendo vya kujiheshimu.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuonesha kwa vitendo njia za kujiheshimu zinazokubalika katika jamii? | 4 |
| b) Kupenda na Kuwaheshimu Watu. | Mwanafunzi aweze kuonesha kwa vitendo tabia njema za kuwaheshimu watu. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha kwa vitendo tabia njema za kuwaheshimu watu. | 1. Picha zinazoonesha heshima kwa watu.<br>2. Picha mguso.<br>3. Kitabu cha kiada.<br>4. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je mwanafunzi anaweza kuonesha kwa vitendo tabia njema za kuwaheshimu watu? | 5 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Upendo kwa Watu. | Mwanafunzi aweze kuonesha tabia njema za upendo kwa watu. | Kwa kutumia mbinu ya burudiko, mwalimu awaongoze wanafunzi kuimba wimbo unaofuatana na vitendo vinavyoonesha tabia njema za upendo kwa watu. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kuonesha tabia njema za upendo kwa watu? | 5 |
| **8. MZANZIBARI NA MTANZANIA**<br>a) Mzanzibari na Vitu Vinavyomtambulisha | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya Mzanzibari. | Kwa kutumia mbinu ya utafiti sahili, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya Mzanzibari. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je mwanafunzi anaweza kueleza maana ya Mzanzibari? | 10 |
| | (ii) Kutaja vigezo vinavyomtambulisha kuwa Mzanzibari. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi ikisaidiwa na vielelezo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vigezo vinavyomtambulisha kuwa Mzanzibari. | 1. Vitambulisho vya Mzanzibari.<br>2. Cheti cha kuzaliwa. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vigezo vinavyomta-mbulisha kuwa Mzanzibari? | |
| b) Mtanzania na Vitu Vinavyomtambulisha. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya Mtanzania. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya Mtanzania. | 1. Kitabu cha kiada.<br>2. Kitabu cha kiada katika maandishi ya Braille. | Je,mwanafunzi anaweza kueleza maana ya Mtanzania? | 10 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kutaja vigezo vinavyomtambulisha kuwa Mtanzania. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi ikisaidiwa na vielelezo, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja vigezo vinavyomtambulisha kuwa Mtanzania. | 1. Vitambulisho vya Mzanzibari na Mtanzania, cheti cha kuzaliwa, hati ya kusafiria. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja vigezo vinavyomtambulish a kuwa Mtanzania? | |
| 9. HAKI NA WAJIBU WA MTOTO. Vitendo Vizuri vya Kufanyiwa Mtoto Nyumbani. | Mwanafunzi aweze: (i) Kubainisha vitendo vizuri anavyostahili kufanyiwa mtoto akiwa nyumbani. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha vitendo vizuri anavyostahili kufanyiwa mtoto akiwa nyumbani. | 1. Chati inayoonesha haki za mtoto . 2. Chati mguso inayoonesha haki za mtoto. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha vitendo vizuri anavyostahili kufanyiwa mtoto akiwa nyumbani? | 9 |
| | (ii) Kuyatekeleza matendo mazuri akiwa nyumbani | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kuyatekeleza matendo mazuri akiwa nyumbani. | Vifaa vinavyotumika kufanyia igizo. | Je, mwanafunzi anaweza kuyatekeleza matendo mazuri akiwa nyumbani? | |

## DARASA LA PILI

### UJUZI

Baada ya kujifunza somo la Sayansi Jamii katika Darasa la II wanafunzi wataonesha ujuzi wa:

1. Kuelezea historia ya koo zao na kulinganisha uhusiano wa wanakoo wa zamani na sasa.
2. Kueleza muundo wa uongozi wa skuli na kuheshimu viongozi wake.
3. Kushiriki katika kuongoza na kuchagua viongozi wa skuli.
4. Kuainisha na kueleza sifa za Mzanzibari na Mtanzania.
5. Kubainisha na kueleza mambo yanayounda utamaduni wa Mzanzibari na Mtanzania.
6. Kueleza mambo yanayohatarisha usalama wao barabarani na kutumia barabara kwa uangalifu.
7. Kuhifadhi, kusafisha na kutumia mazingira yao kwa njia endelevu.
8. Kubainisha na kutetea haki zao katika skuli pamoja na kutekeleza wajibu wao.
9. Kutumia maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kisayansi jamii.
10. Kubainisha na kuepuka mambo yanayohatarisha usalama wao ndani ya jamii.

### MALENGO

Malengo ya kufundisha somo la Sayansi Jamii katika Darasa la II ni kuwezesha wanafunzi:

1. Kufahamu masimulizi ya chimbuko la koo zao na uhusiano wa wanakoo hapo kale na sasa.
2. Kuvitambua vitu vilivyomo katika mazingira yao na kufahamu utunzaji wa mazingira hayo.
3. Kutambua mambo yanayohatarisha usalama wao katika maisha ya kila siku na uepukaji wake.
4. Kuwa watulivu, wenye utii kwa uongozi, wenye kujiheshimu na kuwaheshimu wengine.
5. Kutambua utamaduni wa Taifa lao, kuthamini na kudumisha utamaduni unaofaa.
6. Kutambua na kuheshimu uongozi wa skuli.
7. Kufahamu haki zao na wajibu wao wakiwa skuli kama mwanafunzi.
8. Kupata stadi ya matumizi ya maktaba na vifaa vya TEHAMA ili kupata maarifa na stadi za kisayansi.

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **1. FAMILIA YETU, UKOO WETU**.<br>a) Maana ya Ukoo. | Mwanafunzi aweze:-<br>(i) Kueleza maana ya ukoo. | Kwa kutumia mbinu ya mhadhara mfupi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya ukoo. | 1. Chati inayoonesha muundo wa ukoo.<br>2. Chati mguso inayoonesha muundo wa ukoo. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya ukoo? | 8 |
| | (ii) Kutaja koo zao. | Kwa kutumia mbinu ya utafiti sahili, mwalimu awaongoze wanafunzi kutaja koo zao. | 1. Chati inayoonesha muundo wa wanaukoo.<br>2. Chati mguso inayoonesha muundo wa wanakoo. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja ukoo wake? | |
| b) Chimbuko la Ukoo Wetu. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza chimbuko la ukoo wake. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza chimbuko la ukoo. | 1. Chati inayoonesha muundo wa wana ukoo.<br>2. Chati mguso inayoonesha muundo wa wana ukoo. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza chimbuko la ukoo wake? | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | ZANA/VIFAA | UPIMAJI | VIPINDI |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | (ii) Kubainisha Manufaa ya Ukoo. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha manufaa ya ukoo. | 1. Chati inayoonesha muundo wa ukoo.<br>2. Chati mguso inayoonesha muundo wa ukoo. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha manufaa ya ukoo? | |
| | (iii) Kuchora mchoro unaoonesha wana ukoo. | Kwa kutumia mbinu ya mchoro, mwalimu awaongoze wanafunzi kuchora mchoro unaoonesha wanaukoo. | 1. Chati inayoonesha muundo wa ukoo.<br>2. Chati mguso inayoonesha muundo wa ukoo. | Je, mwanafunzi anaweza kuchora mchoro unaoonesha wanaukoo? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| c) Mashirikiano Baina ya Wanaukoo Zama za Kale. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza wanaukoo walivyoshirikiana zama za kale. | Kwa kutumia mbinu ya kujisomea maktaba, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza wana ukoo walivyoshirikiana hapo zama za kale | 1. Vitabu vinavyoeleza mashirikiano ya wanaukoo zama za kale.<br>2. Vitabu vyenye maandishi ya Braille vinavyoeleza mashirikiano ya wana ukoo zama za kale. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza wanaukoo walivyoshirikiana zama za kale? | 8 |
| | (ii) Kueleza wana ukoo wanavyoshirikiana hivi sasa. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza jinsi wana ukoo wanavyoshirikiana hivi sasa. | 1.Chati inayoonesha wanaukoo wanavyoshirikiana hivi sasa<br>2.Chati mguso ya wanaukoo wanavyoshirikia-na hivi sasa. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza jinsi wanaukoo wanavyoshirikiana sasa? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **2. SKULI YETU**.<br>a) Maendeleo ya Skuli. | Mwanafunzi aweze kueleza hatua za maendeleo ya skuli yake. | Kwa kutumia mbinu ya utafiti sahili, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza hatua za maendeleo ya skuli yao. | 1.Mafaili yenye kumbukumbu za maendeleo ya skuli yao.<br>2.Taarifa za kumbukumbu za maendeleo ya skuli yao katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza hatua za maendeleo ya skuli yake? | 4 |
| b) Sheria za Skuli. | (i) Kueleza baadhi ya sheria za skuli yake. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza baadhi ya sheria za skuli. | 1.Chati mguso inayoonesha baadhi ya sheria za skuli.<br>2. Chati mguso. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza baadhi ya sheria za skuli yake? | 10 |
| | (ii) Kutekeleza sheria za skuli yake. | Kwa kutumia igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha namna ya kutekeleza sheria za skuli. | Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kutekeleza sheria za skuli? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| **3.UTAMADUNI WA MZANZIBARI** Vipengele vya Utamaduni wa Mzanzibari. | Mwanafunzi aweze :<br>(i) Kueleza maana ya utamaduni. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya utamaduni. | 1.Mazingira halisi.<br>2.Kanda za kunasia sauti. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya utamaduni? | 13 |
| | (ii) Kubainisha vipengele vya utamaduni wa Mzanzibari. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha vipengele vya utamaduni wa Mzanzibari. | 1.Orodha inayoonesha vipengele vya utamaduni wa Mzanzibari.<br>2. Mazingira halisi.<br>3. Orodha ya vipengele vya utamaduni wa Mzanzibari katika maandishi ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha vipengele vya utamaduni wa Mzanzibari? | |
| 4.MAZINGIRA YETU. Shughuli za Kiuchumi | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kubainisha shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo, mwalimu awaongoze wanafunzi kubainisha shughuli za | 1. Chati inayoonesha shughuli za kiuchumi | Je, mwanafunzi anaweza kubainisha shughuli za kiuchumi | 12 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| Zinazofanyika katika Mazingira. | mazingira ya Zanzibar. | kiuchumi zinazofanyika katika mazingira ya Zanzibar. | zinazofanyika katika mazingira ya Zanzibar.<br>2. Chati mguso inayoonesha shughuli za kiuchumi zinazofanyika katika mazingira ya Zanzibar.<br>3. Mazingira halisi. | zinazofanyika katika mazingira ya Zanzibar? | |
| | (ii) Kueleza manufaa ya kila shughuli ya kiuchumi inayofanyika katika mazingira ya Zanzibar. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza manufaa ya kila shughuli ya kiuchumi inayofanyika katika mazingira ya Zanzibar. | Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza manufaa ya kila shughuli ya kiuchumi inayofanyika katika mazingira ya Zanzibar? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| 5. **USALAMA.** Mambo Yanayohatarisha Usalama Ndani ya Jamii. | Mwanafunzi aweze: (i) Kutaja mambo yanayohatarisha usalama ndani ya jamii. | Kwa kutumia mbinu ya bungua bongo mwalimu awaongoze wanafunzi kuonyesha mambo yanayohatarisha usalama ndani ya jamii. | 1. Picha inayoonesha mazingira hatarishi.<br>2.Picha mguso inayoonesha mazingira hatarishi. | Je, mwanafunzi anaweza kutaja mambo yanayohatarisha usalama ndani ya jamii? | 10 |
| | (ii) Kuepuka mambo yanayohatarisha usalama ndani ya jamii. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha namna ya kuepuka mambo yanayohatarisha usalama ndani ya jamii. | Mazingira halisi | Je, mwanafunzi anaweza kuepuka mambo yanayohatarisha usalama ndani ya jamii? | |
| 6**. UZALENDO**.<br>a) Heshima na Utii kwa Uongozi wa Skuli. | Mwanafunzia aweze: (i) Kueleza uongozi wa skuli yake. | Kwa kutumia mbinu ya majadiliano ya vikundi, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza uongozi wa skuli yao. | 1. Chati inayoonesha muundo wa uongozi wa skuli.<br>2. Chati mguso inayoonesha | Je, mwanafunzi anaweza kueleza uongozi wa skuli yake? | 14 |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | muundo wa uongozi wa skuli. | | |
| | (ii) Kutekeleza sheria na taratibu za skuli. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha jinsi ya kutekeleza sheria na taratibu za skuli. | 1. Mazingira halisi.<br>2. Chati inayoonesha sheria na taratibu za skuli.<br>3. Chati mguso inayoonesha sheria na taratibu za skuli. | Je, mwanafunzi anaweza kutekeleza sheria na taratibu za skuli? | |
| | (iii) Kuonesha heshima kwa uongozi wa skuli. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha namna ya kuonesha heshima kwa viongozi wa skuli. | Mazingira halisi. | Je, mwanafunzi anaweza kuonesha heshima kwa uongozi wa skuli? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
| b) Heshima na Utii kwa Uongozi wa Shehia. | Mwanafunzi aweze:<br>(i) Kueleza maana ya Shehia. | Kwa kutumia mbinu ya maswali na majibu mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza maana ya Shehia . | 1. Maandiko yanayohusu muundo wa utawala Zanzibar.<br>2. Maandiko ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kueleza maana ya Shehia? | 16 |
| | (ii) Kutekeleza kazi na wajibu wa mamlaka ya Shehia. | Kwa kutumia mbinu ya kualika mgeni, mwalimu awaongoze wanafunzi kueleza kazi na mamlaka ya uongozi wa Shehia. | 1. Maandiko kuhusu kazi za wakuu wa Shehia.<br>2. Maandiko ya Braille. | Je, mwanafunzi anaweza kutekeleza kanuni za uongozi wa Shehia? | |
| | (iii) Kuonesha heshima kwa uongozi wa Shehia. | Kwa kutumia mbinu ya igizo dhima, mwalimu awaongoze wanafunzi kuonesha namna ya kuheshimu uongozi wa Shehia. | Vifaa vinavyotumika kufanyia igizo. | Je,mwanafunzi anaweza kuonesha namna ya kuheshimu uongozi wa Sheria? | |

| MADA KUU/ MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA / KUJIFUNZIA | VIFAA/ZANA | UPIMAJI | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|---|
